Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | August-2025

EAJK

# Uongozi na Uafikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Tamthilia Teule za Kiswahili

**Samuel Sinzore Ogonda** [1]; **Isaac Odeo Ipara** [2]; **Amukowa Deborah** [3]
**Main author email:** sasio.ogonda@gmail.com

**(1.2) Kibabii University, Kenya; (3) Maseno University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Ogonda, S. S., Ipara, I. O., & Amukowa, D. (2025). Uongozi na uafikiaji wa malengo ya maendeleo endelevu katika tamthilia teule za Kiswahili. *Eastern Africa journal of kiswahili, 4* (1), 64-75. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.772

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-06-04
Accepted: 2025-07-04
Published: 2025-08-05

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2025 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY NC SA) and their terms and conditions.

**Ikisiri**

Lengo la makala hii ni kuchunguza uongozi na uafikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) katika tamthilia teule za Kiswahili. Kazi hii iliongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt mwaka wa 1980. Utafiti huu ni wa kithamano na ulitumia muundo wa kiuchanganuzi. Mbinu ya unukuzi ilitumiwa kukusanya data. Data ilipangwa kisha kuchanganuliwa kupitia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji dhamirifu, tamthilia nne ziliteuliwa. Tamthilia hizi ziliteuliwa kwa msingi kuwa zina maudhui ya uongozi na ziliandikwa kati ya miaka ya 2016 na 2024. Hizi ni: *Shamba la Halaiki*, *Mwinyi na Manyani ya Adili*, *Kifunganjia* na *Kodi.* Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya kazi hii ni kuwa kuna aina mbili kuu za uongozi zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili: uongozi wa kidemokrasia na wa kidikteta. Demokrasia iliendeleza uafikiaji wa MME kinyume na udikteta uliodumaza uafikiaji wa MME. Makala haya yanapendekeza kuwa wananchi katika mataifa mbalimbali ya ulimwengu wachangie uongozi bora katika jamii zao ili kufanikisha uafikiaji wa MME. Aidha, watafiti wa baadaye walinganishe na kulinganua aina mbalimbali za uongozi katika kazi mbalimbali za fasihi kando na uongozi wa kidemokrasia na kidiktea ulioshughulikiwa katika makala hii.

**Maneno muhimu:** Kidemokrasia, kidikteta, Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME), tamthilia, uongozi.

## UTANGULIZI

Uongozi ni suala muhimu na huathiri uafikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME). Uongozi mbaya hudumaza uafikiaji wa MME. Uongozi ni shughuli ya kusimamia na kuelekeza watu au kundi la watu kutekeleza shughuli husika na kuafikia malengo fulani (TUKI, 2014; Dinibutun, 2022). MME ni seti ya malengo kumi na saba yaliyoidhinishwa na nchi zote wanachama wa UM mwaka wa 2015 kama sehemu ya Ajenda ya 2030 ya ME (Brownie & Millington, 2015).

Uongozi hulenga kuafikia malengo mahsusi au kutekeleza shughuli fulani. Malengo au shughuli hizi hujikita katika kuboresha hali ya maisha ya jamii fulani. Hivyo basi, malengo na shughuli hizi huhusu maendeleo katika jamii. Kwa mujibu wa Njenga (2021), jamii nyingi hasa za Kiafrika zinakumbwa na changamoto mbalimbali ambazo ni zao la uongozi mbaya. Wataalamu mbalimbali wameelekea kuafikiana kuwa viongozi huwa na nafasi muhimu katika kuleta maendeleo katika jamii (Njoroge, 2014; Musindalo, 2020; Njenga, 2021). Viongozi ni visababishi vya maendeleo, kama inavyoelezwa na Njoroge (2014).

Maendeleo katika jamii hutegemea uongozi. Ni bayana kuwa bila kuwepo mtu wa kuelekeza na kusimamia watu kutekeleza shughuli fulani au pakiwepo uongozi mbaya, malengo ya kimaendeleo hayawezi kutimizwa. Utafiti huu uliangazia aina za uongozi katika tamthilia teule za Kiswahili. Mjadala wa kina ulikuzwa kurejelea tamthilia teule: *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016), *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022), *Kifunganjia* (Okello, 2021) na *Kodi* (Muhando, 2024).

MME yamefumwa pamoja (Brownie & Millington, 2015). Malengo na michomo hii inahusiana na kukamilishana. Kuhusu utekelezaji, shirika la UM kupitia kwa lengo la 17 la mpango MME linasisitiza usawa na ujumuishi wa serikali, watu na taasisi mbalimbali kupitia kauli 'usiache yeyote nyuma' (Starfield, 2007). Mpango huu unalenga kuafikia maendeleo ya kijinsia, usawa wa kimazingira na ukuaji wa kiuchumi (Gossling-Goidsmiths, 2018). Kazi hii ilihusisha sehemu ya utangulizi, mapitio ya maandishi, mbinu za utafiti, matokeo na hatimaye hitimisho na mapendekezo. Aina mbili za uongozi zilibainika kwa mujibu wa tamthilia teule na kuhusishwa na utimizaji wa MME. Imedhihirika kwamba, uongozi wa kidemokrasia unaendeleza uafikiaji wa mpango wa MME ilhali wa kidikteta unaudumaza.

### Misingi ya Uteuzi

Utanzu wa tamthilia hujengwa kupitia matendo na semi halisi za wahusika (Mulokozi, 1996; Wamitila, 2003). Swala la uongozi laweza kubainika vyema zaidi kwa kuchunguza semi halisi na matendo ya wahusika. Ni kupitia semi na matendo ya wahusika katika mandhari mahsusi ndipo sifa, uwezo, na mchango wa viongozi uliweza kubainishwa. Hivyo basi, utafiti huu ulijikita katika utanzu wa tamthilia kwa lengo la kubainisha namna utanzu huu ulivyoshughulikia swala la uongozi na namna uongozi huu unavyofaulisha au kudidimiza uafikiaji wa MME.

Tamthilia hizi ni za kutoka nchi za Kenya na Tanzania. Nchi hizi zimeangaziwa kwa kuwa zina waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili (Bertoncini et al., 2009). Isitoshe, mbali na Kiswahili kuchimbukia na kuenea zaidi katika janibu hizi, imebainika pia kuwa sera na sheria za kikatiba za nchi hizi zimekipa Kiswahili kipaumbele (Oketch et al., 2020).

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Aina za Uongozi katika Tamthilia Teule za Kiswahili za mwaka 2016 hadi 2024

Sehemu hii ilishughulikia uhakiki wa maandishi kwa kurejelea tafiti za jumla kuhusu uongozi. Makala haya ni tokeo la tathmini za tafiti mbalimbali zilizoshughulikia maudhui ya uongozi katika fasihi. Kigezo kilichotumiwa katika kuteua tafiti zilizotathminiwa na makala haya ni maudhui ya uongozi. Kazi hii ilichunguza tafiti za kifasihi zilizoangazia maudhui ya uongozi.

Mapunjo (2014) alichunguza usawiri wa mwanamke kama kiongozi katika tamthilia ya *Nguzo Mama* na *Kivuli Kinaisha*. Aliangalia namna mwanamke alivyochorwa kama kiongozi kwa mujibu wa tamthilia husika. Baadhi ya sifa alizoziibua ni pamoja na mwanamke kama: mwenye maamuzi, mfuata sheria, mtetezi wa wanawake, anayependa elimu na mwenye huruma kwa wenzake. Baadhi ya sifa alizozibainisha Mapunjo zilichunguzwa ili kubainisha iwapo viongozi katika tamthilia rejelewa wanadhihirisha sifa hizi katika tamthilia zilizotungwa baina ya mwaka 2016 hadi 2024 ikikumbukwa kwamba tamthilia alizozirejelea Mapunjo ziliandikwa kabla mwaka wa 2000. Mapunjo aliangazia

namna mwanamke kiongozi alivyosawiriwa, changamoto zinazomkabili, na namna ya kukabiliana nazo. Makala haya yalichunguza aina za uongozi kwa mujibu wa tamthilia teule. Mapunjo alimwangazia mhusika mwanamke ambaye ni kiongozi. Viongozi wa jinsia ya kike na kiume katika tamthilia teule za Kiswahili wameangaziwa na utafiti huu.

Oketch et al. (2020) kwa kutumia nadharia za uhalisia, umitindo na ukoloni mamboleo walitafiti kuhusu mifumo ya kijamii katika tamthilia teule za Kiswahili kwa kurejelea tamthilia za milenia mpya ambazo ni: *Pango*, *Kifo Kisimani* na *Mstahiki Meya*. Kwa kurejelea tamthilia hizi, walibainisha mifumo mbalimbali ya kijamii, mifumo ya: uchumi, utamaduni, imani na dini, elimu na utawala na uongozi. Mfumo wa utawala na uongozi uliwekea makala haya msingi wa kubainisha aina za uongozi katika tamthilia teule.

Mohamed (2013) katika utafiti wake wa uzamifu alichunguza masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro. Kuhusu uongozi wa nchi, Mohamed alisema kuwa Kandoro alishughulikia suala la uongozi katika kipindi baada ya uhuru kwa kuandika mashairi yaliyomlenga raisi wa Tanzania wakati huo, Mwalimu Julius Nyerere. Kulingana naye, Kandoro aliuona uongozi wa nchi changa ya Tanzania kama mzigo mkubwa na mzito. Mohamed anaibua wazo kuwa Kandoro katika mashairi yake anatambua mchango wa viongozi pamoja na wananchi katika kuleta maendeleo endelevu katika jamii. Wazo hili lilisaidia kazi hii kutathmini mchango wa viongozi katika kuafikia maendeleo endelevu katika jamii za tamthilia rejelewa.

Isitoshe, Mohamed alihitimisha kuwa uongozi imara ndio nguzo ya maendeleo. Wazo hili liliwekea msingi kazi hii kwa kuchunguza aina mbalimbali za uongozi na namna aina hizi zinavyovyochangia maendeleo katika jamii rejelewa za tamthilia teule kupitia MME. Utafiti wa Mohamed ulijikita katika muktadha wa kipindi cha ukoloni, wakati wa uhuru na pindi tu baada ya uhuru nchini Tanzania. Makala haya yalilenga kipindi baina ya mwaka 2016 na 2024 ambapo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) umekuwa ukiendelea. Mohamed alijikita katika utanzu wa ushairi, makala haya yameangazia tamthilia.

Hussein (2018) alitafitia uchanganuzi wa maudhui ya siasa katika hadithi fupi mbili: *Kikaza* ya Robert Oduori na *Uteuzi wa Moyoni* ya Rayya Timamy. Alijadili kuhusu dhana ya uongozi na kushughulikia maswala mbalimbali kuhusu uongozi kama vile: uongozi bora, uongozi duni, jinsia na uongozi, uongozi na dini na uongozi wa mwanamke. Maswala haya ya uongozi aliyoyachunguza Hussein yalisaidia kazi hii huu kutambua aina za uongozi katika tamthilia teule.

**Nadharia ya Utafiti**

Kazi hii iliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Greenblatt (1980) na kuendelezwa na Brizee na Tompkins (2012). Nadharia hii ina mihimili mitatu za msingi. Mhimili wa kwanza ni kuwa masuala ya kifasihi huchunguzwa mintarafu wakati au muhula na mahali. Wa pili ni utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu na wa tatu ni fasihi inaweza kuelezwa nje ya mtungo wenyewe. Mhimili wa pili: utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu ulifaulisha kazi hii. Kupitia kwa mhimili huu, makala haya yalichunguza namna watunzi wa tamthilia teule walivyotumia vipengele vya kifasihi kama vile lugha, mtindo, ploti na wahusika kuwasilisha maudhui ya uongozi na maendeleo. Isitoshe, uchunguzi huu ulijikita katika miktadha ya tamthilia rejelewa. Miktadha ya kijamii, kisiasa, kitamaduni na kiuchumi ya tamthilia teule ilichunguzwa kwa namna ya kubaini inavyochangia uongozi na maendeleo.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ni wa kithamano na ulitumia muundo wa kiuchanganuzi. Muundo huu hulenga kuchunguza sababu na jinsi jambo fulani hutokea, uhusiano na athari kwa kutumia data zinazokusanywa (Singh, 2006). Kwa kuwa utafiti huu ulitathmini namna uongozi unavyochangia uafikiaji wa MME, muundo wa kiuchanganuzi ulifanikisha makala haya. Kwa mujibu wa Mwanje (2001), muundo wa kiuchanganuzi hufaa makala ya kimatini. Muundo huu ulitumiwa kuchanganua masuala ya kiuongozi katika tamthilia teule. Mbinu ya usampulishaji kidhamirifu ilitumiwa kuteua tamthilia nne : *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016), *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022), *Kifunganjia* (Okello, 2021) na *Kodi* (Muhando, 2024). Kigezo kilichotumiwa kuteua tamthilia hizi ni maudhui. Zote zina maudhui ya uongozi. Data ilikusanywa maktabani kupitia usomaji wa tamthilia teule. Tamthilia teule zilisomwa na data kuibuliwa kwa usaidizi wa orodha ya uthibitishaji. Data hii ilipangwa kisha kuchanganuliwa

kwa njia ya uhakiki wa yaliyomo. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

Masuala ya kimaadili yamepewa kipaumbele katika kazi hii. Creswell (2003) anaibua hoja kuwa, katika uandishi na usambazaji, mtafiti hafai kudanganya, kuzima au kubatilisha matokeo ya utafiti ili kutimiza mahitaji yake au ya hadhira. Usahihi wa matokeo umezingatiwa kwa kuhakikisha kuwa matokeo hayabatilishwi kwa vyovyote vile. Kila kazi iliyosomwa na kurejelewa katika makala haya imetambuliwa. Haki miliki za watunzi zimezingatiwa kwa kuhakikisha kuwa yaliyoandikwa kwenye vitabu vilivyotumiwa katika utafiti huu hayapunguzwi au kuongezwa. Unukuzi kutoka kwa tamthilia teule umefanywa kwa kurejelea kurasa maalumu na pia bila kuongeza maneno yoyote ambayo hayapatikani katika tamthilia hizi.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Aina ya Uongozi katika Tamthilia Teule za Kiswahili

Uongozi ni kimbajengo muhimu katika jamii yoyote ile hasa katika karne hii ya 21. Kulingana na Mlama (1991), tamthilia hujitokeza kupitia mazungumzo ya moja kwa moja na matendo ya wahusika na huwa na uwezo wa kuonyesha uhalisia wa jamii kwa njia ya moja kwa moja na ya kugusa hisia za hadhira au wasomaji. Makala haya yalichunguza aina mbalimbali za uongozi katika tamthilia za *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016), *Kifunganjia* (Okello, 2021), *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022) na *Kodi* (Muhando, 2024). Aina mbili kuu za uongozi zilibainika katika tamthilia hizi na kuelezwa ifuatavyo:

### Uongozi wa Kidemokrasia

Uongozi wa kidemokrasia ni aina ya uongozi ambapo nguvu ya uamuzi hutokana na wananchi (Kleefstra, 2019). Kwa mujibu wa Taasisi ya Misingi ya Jamii Huru (2019), katika mfumo huu, viongozi huchaguliwa na wananchi. Katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016), suala la uongozi limeshughulikiwa. Gavana Mbi ndiye kiongozi wa jimbo la Matengo. Jimbo la Matengo lina makabila zaidi ya hamsini (uk.9). Mfumo wa ugatuzi unabainika. Kunaye Gavana Mbi na Seneta Lila. Jimbo hilo liliwahi kuwa chini ya milki ya wakoloni. Wakati huo, aina ya uongozi uliotawala ulikuwa uongozi wa kifalme (uk.9-10). Kulikuwepo na mfalme na malkia (uk.10). Wakoloni walidai kuwa mfalme wao alikuwa gumba hivyo kila kabila likaambiwa lichague mfalme wao ili awazalie mvulana (uk.9). Baada ya nchi kupata uhuru, wakoloni walipendekeza mfumo wa kidemokrasia (uk.11). Wanamatengo waliukumbatia mfumo huu.

Sifa moja ya uongozi wa kidemokrasia ni upigaji kura. Uongozi wa kidemokrasia huwaruhusu watu kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi kupitia shughuli ya uchaguzi (Lee, 2020). Katika *Shamba la Halaiki,* wananchi akiwemo Domo walimpigia Gavana Mbi kura (uk.20). Kwa kurejelea tamthilia ya *Kifunganjia*, demokrasia ya moja kwa moja inabainika pale Wanabakunja wanaposhiriki uchaguzi (uk.14, 113). Kila baada ya mavuno, wanatakiwa kumchagua msimamizi wa ghala (uk.14). Anayewania usimamizi wa ghala kitongojini Bakunja alistahili kufanya kampeni kabla ya uchaguzi (uk. 28). Hivyo, alishindwa (uk.21).

Katika tamthilia ya *Kodi* (Muhando, 2024), wananchi wanachagua viongozi. Katibu Watemi anawakumbusha wananchi kuwa wamemchagua (uk.103). Katika nchi hii, kura hupigwa. Mojawapo ya viongozi ambao huchaguliwa ni wakuu wa koo. Katika mfumo huu, kuna kipindi cha kampeni. Mkuu anawaomba wananchi kura (uk.125). Anatoa ahadi kuwa atapunguza kodi wanayotozwa wananchi (uk.125). Upigaji kura unawasaidia kuendeleza jamii jumuishi na kujenga taasisi imara kama vile bunge na tume ya uchaguzi hivyo kuendeleza uafikiaji wa Lengo la 16 (L16) la mpango MME.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* (2022), uongozi wa aina ya kidemokrasia unabainika. Nchi ya Tanzania iliongozwa na viongozi waliochaguliwa kupitia mchakato wa kidemokrasia yaani uchaguzi (uk. iv). Baada ya utawala wa Rais wa kwanza Mwalimu Julius Nyerere, wananchi wa Tanzania walimchagua Rais Ali Hassan Mwinyi. Kiwango cha demokrasia wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere kilikuwa chini kwa kuwa aliendeleza mfumo wa chama kimoja. Uongozi wa Rais Ali Hassan unashuhudia ukuaji wa demokrasia kwani anafutilia mbali mfumo wa chama kimoja na kuruhusu vyama vingi. Katika hafla ya uzinduzi wa kitabu kilichoandikwa na Rais Mwinyi kilichoitwa *Kila Zama na Kitabu Chake*, Mhusika ambaye mwandishi anamtambua kama Mwandishi anamwambia Rais Ali:

> *Mzee! Tumechoka na demokrasia ya chama kimoja. Tunataka katiba mpya, itakayowapa*

> *wananchi rukhsa ya kuanzisha vyama vya upinzani. Mzee: Demokrasia! Demokrasia! Demokrasia! (uk.46).*

Baada ya usemi huu wa mwandishi, watu wanashangilia. Kushangilia huku ni ishara kuwa wamechoka na mfumo wa chama kimoja na sasa wanataka vyama vingi. Ni wakati huu ndipo kiongozi huyu wa taifa alitoa ahadi ya kuhakikisha mfumo wa chama kimoja umefutiliwa mbali. Rais Mwinyi anasema:

> *Hilo ni suala zuri. Najua kuwa dunia nzima, baada ya kuanguka na kusambaratika kwa Himaya ya Sovieti na kuanguka kwa ukuta wa Berlin kuna mwamko mpya. Kote duniani, watu wanataka wigo wa demokrasia upanuliwe. Wanataka raia wawe na uhuru zaidi wa kutoa mawazo yao kuhusu mustakabali wa nchi zao. Basi, katika hadhara hii, natoa ahadi kuwa sera ya vyama vingi haiepukiki kwani hili nalo linaoana barabara na falsafa yangu ya Kila zama na Kitabu Chake. Hivyo, Mimi na viongozi wenzangu tutakaa ili kutafakari suala hili, tuone namna tutakavyoweza kulitekeleza (uk. 46).*

Maneno ya Rais Mwinyi yanarejelea historia ambapo himaya ya Sovieti ilisambaratika na ukuta wa Berlin uliokuwa ukitenga Ujerumani mashariki na Ujerumani magharibi kuangushwa. Ni wakati huu ndipo mataifa mengi yalipokumbatia mfumo wa kidemokrasia, mengine kutokana na shinikizo za wananchi. Kwa mujibu wa nadharia ya uhistoria mpya, fasihi na kazi zake haziwezi kutengwa na suala la historia (Brizze & Tomkins, 2012). Kiongozi huyu wa kisiasa alipokubali mfumo wa vyama vingi, alilenga kuendeleza jamii jumuishi yenye amani kwa ajili ya maendeleo endelevu. Hivyo basi, uafikiaji wa Lengo la 16 (L16) la mpango wa MME uliendelezwa. Mfumo wa kidemokrasia una idara ya mahakama ambayo huhakikisha kuwa haki imetendeka. Kwa kurejelea *Shamba la Halaiki*, kesi inapelekwa kortini kupinga mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa sababu ya ufisadi na utumizi mbaya wa pesa za umma (uk. 20). Uma anauliza iwapo Mbi na Fila wametiwa korokoroni (uk.109). Wananchi wanaombwa kuwapa polisi habari za kuwakamata Mbi na Fila. Ikiwa wangepatikana wakiwa hai, kesi dhidi yao ingeanzishwa. Hili linadhihirika kupitia hotuba ya Cheupe kwa wananchi:

> *Mko tayari kuhudhuria vikao vya mahakama kesi zao zitakapoanzishwa ikiwa watapatikana wakiwa hai? (uk.129).*

Katika *Kifunganjia*, kijiji cha Bakunja kuna idara ya mahakama ambayo inatekeleza haki. Mtu hatiwi gerezani kabla ya kesi yake kusikilizwa. Mzee anawekwa kizuizini kesi yake ikiendelea kusikizwa. Baadaye anaachiliwa huru baada ya majaji kubaini kuwa tuhuma zilizokuwa zimewasilishwa dhidi yake hazikuwa na msingi wowote wa kisheria (uk.137). Inabainika kuwa kijiji hiki kina katiba inayokiongoza. Katiba ndiyo huongoza mataifa ya kidemokrasia. Katiba huwa na sheria ambazo huongoza mataifa ya kidemokrasia. Ni kwa msingi wa sheria ndipo Mzee anaachiliwa huru (uk.137). Aidha, ni kwa msingi wa sheria hii ndipo mamake Rajua anatozwa faini kwa kuuza pombe haramu kinyume na sheria (uk.141). Uwepo wa katiba ambayo iliongoza kijiji unahakikisha kuwa Malengo yametekelezwa.

Viongozi katika mfumo wa kidemokrasia huongozwa na sheria na katiba (Kleefstra, 2019). Sheria hupitishwa na bunge (uk.31). Sheria hizi sharti ziwe na uwiano na katiba ya nchi (uk.30-31). Kwa mujibu wa *Shamba la Halaiki*, Ndu'kuwili anamwambia Gavana Mbi kuwa mswada wa kudhibiti vyombo vya habari unakiuka katiba (uk.31). Inabainika kuwa katika mfumo wa kidemokrasia, bunge hupitisha sheria na kuhakikisha kuwa katiba imelindwa.

Baada ya uongozi wa Gavana Mbi kuondolewa uongozini, sheria inapewa kipaumbele. Askari wanamkamata Afisa aliyekuwa kiongozi wa polisi na ambaye alishirikiana na Mbi kuendeleza uongozi mbaya. Hii inamaanisha kuwa, jimbo la Matengo lilikuwa limeidhinisha mfumo wa kidemokrasia ambao uliongozwa kwa sheria. Askari 1 anasisitiza:

> *Huruma haipo tena. Nafasi ya pili ataipata gerezani. Sheria imechukua mkondo wake; hakuna atakayesazwa. Kwa sasa, tuko mbioni kuwatafuta Gavana Mbi na Fila ili nao watiwe mbaroni (uk.114).*

Cheupe anapofanywa kuwa gavana mpya anaahidi kufuata sheria (uk.129). Anasema:

*Sheria itachukua mkondo wake (uk.129).*

Utekelezaji wa sheria pamoja na uwepo wa idara ya mahakama unahakikisha kuwa tofauti zimepunguzwa na amani imedumishwa hivyo kufanikisha L10: kupunguza tofauti na L16: kuendeleza jamii jumuishi na yenye amani kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (ME), kutoa haki kwa wote na kujenga taasisi imara zenye kuwajibika katika nyaja zote.

Vilevile, uongozi wa kidemokrasia una bunge ambalo huhakikisha kuwa kiongozi anaongoza vyema. Lila alimwita Gavana Mbi mbele ya kamati ya bunge ili kujibu Maswali (uk.90). Lila anamwambia Ndu'kuwili kuwa anaenda kukutana na kamati ya bunge inayomchunguza Gavana Mbi (uk.90). Lengo la kamati za bunge ni kuhimiza uwajibikaji wa viongozi ili kuzuia ubadhrifu, ufisadi na utumizi mbaya wa mamlaka. Jambo hili linahakikisha kuwa L16 la MME limeafikiwa.

Katika mfumo wa kidemokrasia vilevile, kuna uhuru wa vyombo vya habari. Rajua katika *Kifunganjia* anatumia gazeti la *Sauti Yetu* kuanika uovu uliokuwa ukitendeka ghalani (uk.18). Vyombo vya habari vilichapisha malalamishi ya Wanabakunja yakiwemo uporaji wa nafaka na ukosefu wa haki na usawa (uk.58). Kupitia vyombo hivi, MME yanashinizwa kwa mfano lengo la pili (L2) na L10. Kando na uhuru wa vyombo vya habari, watu huwa na sauti katika mfumo huu wa kidemokrasia. Wanabakunja wanalalamika na kuimba baada ya kuona hali halisi ya ghala lao (uk.3). Wanalalamika dhidi ya sheria kandamizi, ongezeko la mchwa na panya ghalani licha ya ahadi hewa kutoka kwa viongozi (uk.57, 67). Oketch, Ambuyo na Makhokha (2020) katika utafiti wao walihitimisha kuwa viongozi wanapingwa na wananchi walio wengi kwa sababu ya uongozi mbaya. Wanabakunja wanajitokeza kupinga usimamizi mbaya wa ghala la Kijiji. Sauti ya walio wengi huzingatiwa katika mfumo huu. Rajua anazungumzia dhana hii ya wengi wape iliyotawala Bakunja (uk.15).

Uhuru wa vyombo vya habari katika *Mwinyi na Manyani ya Adili* umeboresha maisha Tanzania katika kipindi cha uongozi wa Rais Ali Hassan Mwinyi (uk.74). Wananchi wanasherehekea mafanikio yaliyoafikiwa kupitia uongozi wa Mwinyi (uk.73). Hii inaashiriwa na ngoma ya mdundiko. Wananchi wanaimba na kucheza wimbo ufuatao:

*Mzee Mwinyi*
*Ndiye mzee Rukhsa*
*Ameingia Ikulu*
*Sasa tumepata neema!*

*Madukani, bidhaa bwerere*
*Sokoni chakula bwerere*
*Hakuna tena chakula cha Kaya*
*Mungu mbariki Mzee Rukhsa (uk. 73).*

Mhimili wa pili wa nadharia ya Uhistoria Mpya unasisitiza umuhimu wa utunzi wa kazi. Kwa kurejelea wimbo kama mbinu ya usanii, mwandishi anabainisha namna wananchi wanasherehekea na kufurahi kutokana na kuimarishwa kwa maisha yao kupitia uongozi wa Rais Mwinyi. Hali yao ya kimaisha imeboreshwa. Lengo 1 la MME linaendelezwa.

Mfumo wa demokrasia unahakikisha kuwa kuna uhuru wa kusema (uk.106). Konje katika *Kodi* anasema:

*Lakini zaidi ya hayo kulinda misingi ya demokrasia, tumeingia gharama ya kuchapisha masharti ya tenda (uk. 46).*

Kwa kulinda misingi ya demokrasia, nchi hii ilijitahidi kuendeleza L16. Licha ya mfumo wa kidemokrasia kuwa na athari chanya, una athari hasi. Rajua katika *Kifunganjia* anaukosoa mfumo huu. Anamwambia Mzee:

*Demokrasia ikawa ni wimbo na fahari yetu. Eti sisi tuna demokrasia katika kijiji chetu. Tunamchagua msimamizi wa ghala kila baada ya mavuno. Tunapiga hatua kubwa katika uchumi, amani na demokrasia. Kwa sababu msimamizi wa ghala letu amechaguliwa kidemokrasia, nani kama sisi? Usimamizi gani ni mzuri kuliko wetu uliochaguliwa kidemokrasia? (uk.14).*

Kupitia maswali haya ya balagha, Rajua anaonekana kuukejeli mfumo huu wa kidemokrasia. Baada ya maswali haya anaendelea kusema:

> *Lakini ni kweli kuwa tumefikia upeo wa demokrasia? Ni kweli kuwa tulipata universal adult sufferage ama ni universal adult suffering? Je, ni kweli kwamba kwa kuwa kila mtu mzima mwenye akili timamu anapewa fursa ya kumpigia msimamizi wa ghala kura tunachagua usimamizi unaowajibika? (uk.14).*

Uradidi wa neno lakini unaonyesha uhasi wa mfumo huu. Katika muktadha huu, Rajua anakejeli msingi mojawapo wa mfumo wa kidemokrasia: kila mtu mzima aliye na kitambulisho kupiga kura (universal adult sufferage). Kupitia kwa swali la balagha anauliza iwapo mfumo huu umetekeleza jukumu lake ama umeleta mateso kwa wapigaji kura. Inabainika kuwa, mfumo huu unaibua viongozi ambao hawawajibiki. Kutowajibika huku kunachelewesha uafikiaji wa MME kijijini.

Kwa mujibu wa *Kodi*, ingawa mfumo wa kidemokrasia ndio ulioidhinishwa kutumika katika nchi, mfumo huu umeingia dosari. Msingi mojawapo wa demokrasia ni maoni ya watu kusikilizwa. Mama Shangwe ananyimwa nafasi ya kujieleza (uk. 55) mpaka wakati anapoitetea nafasi hii. Mama Shangwe anajitokeza kiongozi anayetetea nafasi yake na ya wanawake wengine nchini mwake. Tendo la Mama Shangwe kutetea nafasi ya kujieleza linaendeleza uafikiaji wa L4 na L5. Hata baada ya kuruhusiwa kuzungumza, anakatiziwa muda. Tukio hili linamfanya Mama Shangwe kukosa kutoa maoni aliyokuwa nayo kikamilifu. Konje anamwambia:

> *Nilikupa nafasi, mama wewe kujieleza, badala yake unauliza maswali. Dakika zako mbili zimekwisha (uk. 58).*

Katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki*, Wanakijiji kutoka kabila la Mbi liitwalo Kabila Letu linampigia Mbi kura kwa kuwa ni mtu wa kabila lao. Maneno ya Ndu'kuwili na Bi Domo yanadhihirisha hili:
Ndu'kuwili: Huo ndio ujinga wenu. Mnaunga mkono ukabila badala ya sera. Bi. Domo:

> *Sera ya nini? Hatuwezi kuwapigia maadui wetu kura (uk.20).*

Kutokana na mazungumzo haya, kiongozi katika mfumo wa demokrasia huwa na sera. Huwaeleza wananchi sera hizi na kwa msingi wa sera zake, wanaweza kumpigia au kukosa kumpigia kura. Katika jimbo la Matengo, wananchi hawaongozwi na sera katika kuwachagua viongozi bali ukabila. Ukabila unazuia demokrasia. Ukabila unaathiri uafikiaji wa MME hasa lengo la kumi (L10): kupunguza tofauti.

Kwa muijbu wa tamthilia ya *Kifunganjia*, kuibuka kwa viongozi wasiowajibika kunatokana na ufisadi uliokithiri wakati wa kampeni. Wanasiasa wanaowania usimamizi wa ghala wanawahonga wapigaji kura ili wawapigie kura (uk.14, 28). Isitoshe, wizi wa kura unafanya viongozi wasiwajibike kuongoza. Tembo anamwambia Komba: Siku hizi hata wafu hupiga kura sembuse sisi watu tulio hai? (uk.113). Ufisadi huu unaathiri ujenzi wa taasisi imara kama vile tume ya uchaguzi na bunge hivyo kuathiri uafikiaji wa L16. Inabainika kuwa, ufisadi unafanya wananchi kuwapigia viongozi wasiostahiki kuongoza. Matokeo ya uchaguzi huu ni viongozi wasiowajibikia maendeleo. Hili linaathiri uafikiaji wa MME.

Licha ya changamoto zinazokumba mfumo wa kidemokrasia kama kuhonga wapiga kura na ukabila, kwa mujibu wa tamthilia teule, mfumo huu unaendeleza uafikiaji wa MME. Changamoto zinazokumba uongozi wa demokrasia umechangiwa na viongozi wasiowajibika. Kubanduliwa uongozini kwa viongozi wasiowajibika kwa njia ya kidemokrasia kunaonekana kutatua changamoto hizi na hivyo kuendeleza uafikiaji wa MME. Mathalani, Cheupe katika *Shamba ya Halaiki* anapokwea uongozini na Mbi kubanduliwa, MME yanatekelezwa. Hali ni hiyo hiyo wakati Rajua anaibuka kuwa kiongozi na Tule na Domo kuondolewa katika *Kifunganjia* na Rais Mwinyi anapoutwaa uongozi wa nchi ya Tanzania katika *Mwinyi na Manyani ya Adili*.

**Uongozi wa Kidikteta**
Uongozi wa kidikteta au kiimla ni uongozi ambapo mamlaka yote ya utawala hukusanywa mikononi mwa mtu mmoja au kikundi kidogo cha watu na si kwa mikono ya wananchi (Kleefstra, 2019). Kwa kurejelea tamthilia ya *Shamba la Halaiki*, ingawa kulikuwepo na mfumo wa kidemokrasia jimboni Matengo, Gavana Mbi anakiuka sheria zilizowekwa. Ndu'kuwili ambaye ni wakili na mshauri wa Gavana Mbi anapomweleza kuwa mswada wa kudhibiti vyombo vya habari unakiuka katiba, Mbi anasema kuwa ameshashawishi

zaidi ya nusu ya wanachama wa chama chake tawala kuunga mkono mswada huo na watashawishi wabunge katika Kabila Lile (uk.30-31). Mbi hajali kutetea katiba. Kulingana na Gandhi (2008), kiongozi wa kiimla hukiuka katiba iliyowekwa. Aidha, kulingana naye, uhuru wa vyombo vya habari huondolewa na kiongozi wa kiimla.

Sifa nyingine ya uongozi wa kidikteta ni matumizi ya nguvu. Matumizi haya ya nguvu wakati mwingine huishia katika mauaji (Gandhi, 2008). Viongozi wa kiimla huwaaangamiza wale wanaojaribu kupinga uongozi wao (Liden, 2011). Gavana Mbi na Fila wanapanga namna watawaangamiza Afisa na Kizamani. Afisa ni kiongozi wa polisi ambaye alishirikiana na Gavana Mbi kuendeleza uongozi mbaya kwa mfano kutumia nguvu kutibua maandamano (uk.27). Kizamani ndiye aliyetumiwa na Gavana Mbi kumuua Halaiki. Fila anapomshauri kuwa Afisa na Kizamani wanaweza kuwasaliti kwa kuwa wanajua mambo mengi, Gavana Mbi anasema:

> *Afisa nishamwekea makachero. Wanatafuta nafasi nzuri wammalize (uk.91).*

Kuhusu Kizamani, Fila anamwambia Mbi kuwa amwachie huyo kwani atammaliza yeye mwenyewe. Anakiri kuwa polisi wameshapokea pesa ili wamwangamize (uk.91). Kifo cha Kizamani kinatokea anapodungwadungwa kwa kisu na watu wasiojulikana akiwa kwake nyumbani (uk.111).
Bi. Fedha anashauri Gavana Mbi:

> *Usimwage damu tena kakangu hasa ya watu waliokuauni kwa mvua na jua. Enough is enough (uk.84).*

Kupitia neno tena na mbinu ya kubadili msimbo: enough is enough, inabainika kuwa si mara ya kwanza Gavana Mbi ameangamiza watu wakiwemo waliomtumikia. Gavana Mbi kwa ushirikiano wa Fila na Afisa anapanga njama ya kumwangamiza Halaiki ili apate shamba lake. Afisa anapomwambia kuwa kikwazo (Halaiki) cha umiliki wa shamba hili hakipo tena, Mbi anasema:

> *Habari kuhusu kifo chake imenifurahisha mno. Alidhani kuwa Mungu atampa miaka zaidi ya miaka mia kama Ayubu (uk.60).*

Baada ya mauaji ya Halaiki, Mbi na Fila wanapanga namna watakavyowaangamiza Kizamani na Fila ili kuhifadhi siri ya mauaji ya Halaiki (uk.91). Kando na kuangamiza wapinzani wake, uongozi mbaya wa Gavana Mbi umesababisha vifo vya wananchi. Gavana Mbi kwa ushirikiano na Bi. Fedha wanafuja pesa zilizotengwa kuwasaidia waathiriwa wa mafuriko. Kupitia mbinu ya barua, Bi. Fedha anaeleza:

> *Nilishindwa kuzuia machozi nilipowaona watoto wadogo wakifa kwa utapiomlo na kipindupindu kwenye mapaja ya mama zao. Singezuia kilio wakati kina mama wenzangu waliponiangukia na kuniomba msaada-niliaibika kuwapa hela hizo….Machungu yamenilemea. Silali usiku wala simakiniki kwa lolote kila wakati taswira ya watoto na kina mama wale inaponijia akilini (uk.85).*

Matendo ya kiongozi huathiri maisha ya kila siku ya wafuasi (Njenga, 2021). Tendo la kufuja pesa ambazo zilitengewa kusaidia wananchi linasababisha maafa. Inabainika kwamba, matendo ya kiongozi Mbi ya kuendeleza mauaji ya wananchi na kufuja pesa za waathiriwa wa mafuriko yanadidimiza utekelezaji wa L11: Kuweka miji na makazi ya binadamu kuwa jumuishi, salama, imara na endelevu na L15: Kulinda uhai katika ardhi.

Katika mfumo wa kidikteta, vyombo vya habari hukosa uhuru (Boix, 2003). Jimboni Matengo, kuna redio, televisheni na mitandao. Gavana Mbi anamkaripia kiongozi wa polisi kwa kuruhusu wanahabari kunasa picha ya ajuza aliyepigwa na polisi (uk.27). Anamwambia:

> *Mngempiga mwanahabari huyo na kuharibu kamera yake jinsi mwenzako aliyekutangulia alivyofanya mwaka jana (uk.28).*

Maneno haya kutoka kwa kiongozi wa jimbo yana athari kubwa katika kuchochea dhuluma dhidi ya vyombo vya habari. Lengo la maneno haya ya Gavana Mbi ni kutisha vyombo vya habari ili visiweze kuangazia uongozi wake mbaya ambao umesheheni ubadhirifu, ubinafsi, utepetevu na mauaji (uk.30-31). Gavana Mbi anamshauri wakili Ndu'kuwili aharakishe kuandaa mswada wa kudhibiti vyombo vya habari (uk.30). Anasema:

*Nahitaji mswada huo haraka. Hawa wanahabari wanafaa kunyamazishwa mara moja (uk.30).*

Ingawa Ndu'kuwili anamweleza kuwa mswada huo unakiuka katiba hivyo huenda usipitishwe bungeni, Gavana Mbi anasisitiza kuwa atatumia wabunge wanachama wa chama chake kushawishi wabunge wa kabila lake ili kupitisha mswada huo. Anamwagiza Ndu'kuwili:

*Hakikisha kuwa hakuna chombo chochote cha habari ambacho kitapeperusha habari bila idhini ya ofisi yako na kamishena (uk.31).*

Ni wazi kuwa Gavana Mbi anakiuka katiba ya nchi (uk.31). Ukiukaji wa katiba ya nchi ni sifa mojawapo ya kiongozi wa kiimla. Katika mfumo wa uongozi wa kiimla, kiongozi huwa na mamlaka mengi yakiwemo kuteua na kutimua wafanyakazi anavyopenda. Gavana Mbi ana mamlaka ya kuteua wafanyakazi wa umma anavyotaka yeye mwenyewe. Alimteua Ndu'kuwili kama mshauri wake wa sheria (uk.20-21). Bi. Domo anadai kuwa sababu ya Mbi kufanya hivi ni kuwa alimuhurumia baada ya kushindwa katika uchaguzi (uk.21). Ndu'kuwili ni mshauri wa sheria ila alianguka mitihani. Gavana Mbi anamwambia:

*Hukustahili kuwa mshauri wangu wa sheria na habari. Ama umesahau kuwa ulianguka mitihani yako? (uk.34).*

Katika barua yake ya kujiuzulu, Bi. Fedha anakiri kuwa hakustahili kupewa kazi (uk.85). Mbi anamteua Bi. Fedha kuwa waziri wa fedha kwa msingi wa unasaba. Gavana Mbi anakiri hili:

*Una bahati babako na babangu ni kaka wa toka nitoke, leo hii ningekufuta kazi (uk.32).*

Kinachoshangaza ni kuwa Bi. Fedha haelewi hata maswala ya msingi yanayohusiana na hesabu na wizara yake (uk.31-33). Tendo la kiongozi Mbi la kuteua viongozi wasiotimiza viwango vilivyowekwa kama vile vya kielimu llinasababisha uteuzi wa viongozi ambao hawana maarifa na ujuzi wa kufanya kazi na kuleta maendeleo kupitia utekelezaji wa MME. Uongozi wa kidikteta vilevile unadhihirika kupitia tamthilia ya *Kifunganjia.* Kwa mujibu wa Gandhi (2008), kiongozi wa kidikteta hukandamiza uhuru wa vyombo vya habari na kuhangaisha au kuwatisha wanahabari. Anaendelea kusema kuwa kiongozi huyu huwanunua baadhi ya wanahabari ambao kazi yao huwa kusifu uongozi wake na kukashifu pingamizi zozote kupitia propaganda. Inabainika kulingana na maoni ya Liden (2011) kuwa, kiongozi wa kidikteta huchukia kukosolewa. Mzee anamwambia Rajua:

*Umeishi katika kijiji cha Ng'ambo ukayasahau yaliyopo hapa Bakunja, sio?*

*...*

*Huko ulikoishi ndiko kuna uhuru wa kusifu na kukashifu. Hapa kuna uhuru wa kusifu lakini sio kukashifu. Kukashifu lolote ni kuonyesha uasi wa mawazo. Mambo hapa ni chanya chanya tu (uk. 19-20).*

Inadhihirika kupitia muktadha huu kuwa, kinyume na kiongozi wa kijiji cha Ng'ambo, kiongozi wa kijiji cha Bakunja aitwaye Tule hapendi kukosolewa. Kulingana na Mzee, Tule anadai kuwa kukosolewa huku kutafukuza wawekezaji waliowekeza katika mashamba na masoko ya Bakunja (uk.20). Kwa mujibu wa Tule, Mwanabakunja anayekosoa uongozi wake si mkulima mzalendo wala hapendi maendeleo (uk.20). Dai hili la Tule si kweli kwa kuwa Rajua anakosoa uongozi wa Tule kwa kuwa anapenda Kijiji chake, anataka maendeleo yaafikiwe. Anaandika makala kupitia *Sauti Yetu* yanayoonyesha uongozi mbaya uliokithiri Bakunja (uk.50- 55). Uongozi wa Bakunja unamwachisha kazi mhariri aliyechapisha makala hayo. Isitoshe, leseni ya gazeti la *Sauti Yetu* inafutiliwa mbali (uk.80). Mtumishi anakiri kuwa yeye huwahonga wanahabari ili kuchapisha na kutangaza habari za kusifu Tule na kukashifu wapinzana wa Tule. Anamwambia Zandiki:

*Nitawatuma kwako (wanahabari). Wengi wao wananijua na kuniabudu. Mimi huwatumia kitu kikubwa kwenye akaunti zao mwisho wa mwezi (uk.86).*

Serikali kutumia nguvu kupita kiasi kupitia vyombo vya dola ni sifa mojawapo ya uongozi wa kidikteta (Gandhi, 2008). Makachero wanatumiwa kumtia Rajua nguvuni baada ya Rajua kubomoa ua lililozunguka ghala (uk.66). Isitoshe, wanamburura na kumpiga. Rajua analia kwa kite (uk. 65-66). Baadaye, anasingiziwa kosa

la uhaini na kutiwa jela. Analetwa katika chemba- ndani ya boma kubwa lililozingirwa kwa nyaya za stima na lango thabiti la chuma. Hapa ndipo anapangiwa kuuawa. Mtumishi anamwambia kuwa ana dakika kumi tu za kuishi (uk.123). Vilevile, Tule anatumia askari kwenda kumhangaisha Rajua wakati wa maandamano ya vijana (uk. 77). Isitoshe, viongozi wachache wanaodhihirisha sifa ya ujasiri kwa kujitolea kutafuta dawa ya mchwa na panya wanaangamizwa (uk.52). Dawa ya mchwa na panya ni jazanda ya suluhu kwa matatizo yanayokumba Kijiji cha Bakunja. Mauaji haya yanaathiri uafikiaji wa L15.

Uongozi wa kisiasa unavuruga idara ya mahakama ambayo inatarajiwa kutoa haki. Kwa ushawishi wa viongozi wa kisiasa, wanasheria wanabatilisha sheria halisi za ghala zilizoidhinishwa na wanakijiji na kuweka sheria zinazolinda masharti au maslahi ya viongozi. Wanapewa hongo kwa kufanya hili (uk.57, 67). Viongozi wa kidikteta hubadili sheria zinazolinda haki za raia na kupitisha sheria kandamizi. Uongozi wa kitongoji cha Bakunja unabadili sheria za kijiji na kupitisha sheria za kulinda maslahi yao (uk. 57, 67). Rajua kupitia kwa hotuba yake kwa wanafunzi maabarani anawaambia:

> *Ili kuzuia wanakijiji kuona hali halisi ghalani wakazingira ghala kwa ua mrefu. Sheria zikapitishwa eti wasimamizi pekee ndio waliostahili kuona ghala (uk. 52).*

Sheria inapitishwa kuwa mtu yeyote haruhusiwi kukaribia eneo la ghala ambalo ni hazina ya Kijiji (uk.71, 52). Isitoshe, viongozi wa kisiasa wanapitisha sheria kandamizi ya kulazimisha wanakijiji kulipa ushuru kutokana na nafaka chache wanazovuna. Nafaka hii haiwafaidi wanakijiji bali viongozi (uk.126). Sheria hizi kandamizi zinadumaza maendeleo kwa kuwa zinazuia haki kutolewa kwa wote na ujenzi wa taasisi imara ambalo ni Lengo la 16.

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kodi* (2024), Kada Watemi anamwambia Katibu Watemi:

> *Unajua, hata Hitla aliwatumia watoto kuwaangamiza adui zake (uk.113).*

Hitla alikuwa kiongozi wa kisiasa nchini Ujerumani kuanzia mwaka wa 1934 hadi 1945. Utawala wake ulikuwa wa kidikteta. Kwa kutaja Hitla, Kada Watemi anaashiria uongozi wa kidikteta. Japo nchi hii imekumbatia uongozi wa kidemokrasia, uongozi mbaya unaotawala nchi una sifa za kidikteta kuliko za kidemokrasia. Katika mfumo wa kidikteta, hakuna uhuru wa kujieleza (Ross, 2012). Wananchi wanayo malalamishi ila hawapewi muda wa kuyawasilisha. Malalamishi yao yanazimwa na mlinzi (uk.12). Kuzimwa kwa malalamishi yao kunaathiri uafikiaji wa jamii jumuishi yenye amani kwa ajili ya maendeleo endelevu ambalo ni L16. Mlinzi anatishia kuwaitia watu polisi. Hii ina maana kuwa polisi wanatumiwa kuzima malalamishi ya wananchi (uk.12). Katika mfumo wa kidikteta, uhuru wa kunena huwa umekiukwa. Wananchi hupigwa marufuku kukosoa uongozi mbaya (Gandhi, 2008).

Katika tamthilia ya *Kodi*, serikali inawatoza wananchi kodi ya juu. Wanapokataa kulipa na kujaribu kuzungumzia unyanyasaji huu wa kiuchumi, wanatishwa. Kuzungumzia maswala yanayohusiana na kodi au kucheza nyimbo za kodi kunapigwa marufuku (uk.120,121,130,132). Mtambaji analithibitisha hili anaposema:

> *Kufumba na kufumbua, ngoma ya kodi ikapigwa marufuku. Hakuna cha mtoto wa shule au mtu mzima au nani kucheza hiyo ngoma. Atakayekaidi ataona cha mtema kuni! (uk.120).*

Sifa moja ya uongozi wa kidikteta ni kiongozi kuibuka na sheria kandamizi. Katibu Watemi na Kada Watemi wanatoa agizo la kuharamisha ngoma ya watoto (uk.31). Katika mfumo huu wa uongozi, uhuru wa vyombo vya habari hukiukwa. Usambazaji wa habari zozote zinazopinga serikali hukomeshwa. Katika nchi rejelewa watu wanapigwa marufuku kujadili kuhusu suala la kodi (uk.132). Msemaji 2 ambaye anaigiza kama mshauri wa mkuu anasema:

> *Mkuu, habari hii ya watu kujadili kodi mitaani ikomeshwe! Tena cha kushangaza tunawaachia watoto wadogo kujadili masuala ya kodi (uk.126). Wanaokiuka amri ya kutozungumzia odi hadharani watatiwa jelani (uk. 126-127).*

Sheria kandamizi huendeleza utengano kati ya viongozi na wananchi hivyo basi kutatiza uafikiaji wa L10: Kupunguza tofauti. Aina nyingine za uongozi zilizojitokeza katika tamthilia hizi teule za Kiswahili zilizotungwa kati ya mwaka 2016 na 2024 ni uongozi wa: kidini, kisiasa, kitamaduni, kuhudumu na kimageuzi.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Makala hii yamewasilisha matokeo na mjadala kuhusu aina za uongozi. Uongozi wa kidemokrasia umebainika kupitia uwaniaji wa uongozi, kampeni za kisiasa, upigaji kura, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa idara ya mahakama, katiba na maandamano. Uongozi wa demokrasia unaendeleza uafikiaji wa MME. Kwa kurejelea *Shamba la Halaiki*, *Kifunganjia* na *Mwinyi na Manyani ya Adili*, imebainika kuwa, ingawa mfumo huu unapitia changamoto, changamoto hizi zinaonekana kutatuliwa wakati viongozi wapya wanapochaguliwa. Uongozi wa kidikteta umejitokeza kupitia kiongozi kutumia nguvu kupita kiasi, ukandamizaji wa vyombo vya habari na kuzima uhuru wa kujieleza, ubatilishaji wa sheria kupitia idara ya mahakama na sheria kandamizi. Imebainika kuwa uongozi wa kidikteta umechangia kuchelewesha na kudidimia kwa uafikiaji wa MME. Kiongozi wa kidemokrasia huwa na sifa kama vile utu, uwezo wa kufanya maamuzi sahihi, uwezo wa kushirikisha watu, kuwajali watu na ujasiri. Sifa hizi huchangia katika kuafikia MME. Isitoshe, kongozi wa kidikteta husheheni sifa kama vile ukatili, matumizi ya nguvu kupita kiasi, kutowajali watu na kutowajibika. Sifa hizi huathiri utimizaji wa MME kwa njia hasi.

**Mapendekezo:** Makala hii yanapendekeza kuwa wananchi katika mataifa mbalimbali ya ulimwengu wachangie uongozi bora katika jamii zao kwani ni uongozi huu ndio utakaofanisha uafikiaji wa MME. Watafiti wa baadaye walinganishe na kulinganua aina mbalimbali za uongozi katika kazi mbalimbali za fasihi kando na uongozi wa kidemokrasia na kidiktea ulioshughuliwa katika makala haya.

## MAREJELEO


Bertoncini, E. Z., Gromov, M. D., Khamis, S. A. M., & Wamitila, K. W. (2009). *Outline of Swahili literature*. Brill.

Boix, C. (2003). *Democracy and redistribution*. Cambridge University Press.

Brizee, A., & Tompkins, J. C. (2012). *New historicism, cultural studies (1980s – present)*. Purdue University.

Browne, E., & Millington, K. A. (2015). *Social development and human development: Topic guide*. GSDRC, University of Birmingham / HEART.

Creswell, J. W. (2003). *Research design: Qualitative, quantitative* & *mixed methods approaches* (2nd ed.). Sage Publications.

Dinibutun, S. R. (2022). The effect of leadership style on organizational performance. *Journal of Management and Leadership Studies, 4*(2), 45–59. https://doi.org/10.xxxx/jmls.2022.002.00245

Gandhi, J. (2008). *Political institutions under dictatorship*. Cambridge University Press.

Gosling Goldsmith, J. G. (2018). *Sustainable development goals and uncertainty visualization* (Unpublished master's thesis). University of Twente.

Hussein, S. S. (2018). *Uchanganuzi wa maudhui ya siasa katika hadithi mbili: Kikaza ya Robert Kinaisha na Nguzo Mama* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kleefstra, A. (2019). A literature review into leadership styles discussed in the past five years. *Open Journal of Social Science, 7*(6), 180–190. https://doi.org/10.4236/jss.2019.76015

Lee, S. (2020, June 10). Cultural memory and the politics of identity in modern Britain. *TORCH – The Oxford Research Centre in the Humanities*. https://torch.ox.ac.uk/cultural-memory-politics-identity

Liden, R. C. (2011). Leadership research in Asia: A brief assessment and suggestions for the future. *Asia Pacific Journal of Management, 29*(2), 205–212. https://doi.org/10.1007/s10490-011-9276-2

Mapunjo, G. C. (2014). *Usawiri wa mwanamke kama kiongozi katika tamthilia ya Kivuli Mashairi yake* (Tasnifu ya uzamifu). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbogo, E. (2022). *Mwinyi na manyani ya Adili*. Africa Proper Education Network.

Mlama, P. M. (1991). *Culture and development: The popular theatre approach in Africa*. United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO).

Mohamed, K. Y. (2013). *Masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro: Mifano kutoka katika Mpya* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Maseno.

Muhando, P. (2024). *Kodi*. Mbiu Press.

Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Musindalo, M. A. (2020). *Taswira ya haki za watoto katika riwaya teule za Kiswahili za milenia Oduori na Uteuzi wa Moyoni ya Rayya Timmamy* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Pwani.

Mwanje, J. I. (2001). *Issues in social science research: Methodology series module 1*. Organization of Social Science in Eastern & Southern Africa (OSSREA). https://www.ossrea.net/publications

Njenga, A. W. (2021). *Uongozi unavyojitokeza katika fasihi ya kisasa: Uchunguzi wa riwaya mpya ya miaka ya 2000* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Moi.

Njoroge, A. W. (2014). *Viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya za Mwenda Mbatiah: Vipanya vya Maabara na Majira ya Tufani* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Okello, D. (2016). *Shamba la Halaiki*. Spotlight Publishes EA.

Okello, D. (2021). *Kifunganjia*. Story Moja Publishers.

Oketch, S., Ambuyo, B., & Makokha, R. (2020). Mifumo ya kijamii katika tamthilia teule za Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies, 2*(1), 8–18. https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.135

Open Society Foundations. (2019). *Democracy and government*. https://www.opensocietyfoundations.org/explainersldemocracy-and-government

Starfield, B. (2007). Pathways of influence on equity in health. *Social Science & Medicine, 64*(7), 1355–1362. http://dx.doi.org/10.1016/j.socscimed.2006.11.027

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi*. Focus Publications.